
## HUDUMA YA WAJAWAZITO


### Upatikanaji wa Huduma za afya kwa Mjamzito

Kati ya vituo vyote vinavyotoa huduma za afya, asilimia 85 vinatoa huduma za mjamzito. Miongoni wa taasisi zinazotoa huduma za mjamzito ambapo ni asilimia 75 ya vituo hivyo vinavyotoa huduma ya mama mjamzito kwa siku tano au zaidi katika wiki na asilimia 89 vinatoa huduma ya chanjo ya pepopunda kila siku mahali panapotolewa huduma ya mama mjamzito.

### Matokeo ya Ushauri kwa Wajawazito

Karibu wateja wote wa kliniki ya wajawazito walipatiwa huduma ya vitendo: asilimia 80 kati yao walikiri kufanyiwa vipimo vya shinikizo la damu, asilimia 88 walipimwa uzito na asilimia 96 walipimwa kimo cha mimba. Katika huduma za ushauri kwa mama wajawazito asilimia 75 walipatiwa huduma ya vidonge vya madini chuma au madini ya foliki asidi




## Kudhibiti Maambukizi ya VVU kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto kwenye Vituo vinavyotoa Huduma kwa Wajawazito

Miongoni mwa vituo vinavyotoa huduma ya wajawazito, asilimia 94 vinatoa huduma yoyote ile ya kudhibiti maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto. Takriban vituo 9 kati ya 10 vinavyotoa huduma ya wajawazito na huduma yoyote ya Kudhibiti Maambukizi ya VVU kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto vinatoa huduma ya dawa za ART kwa wajawazito wenye VVU.

Takriban vituo vyote vina uwezo wa kupima VVU (93%) kwa watu wazima, wakati asilimia 57 tu huandaa matone ya damu kavu kwa ajili ya kuwapima watoto wachanga. Zaidi ya vituo 7 kati ya 10 vina dawa aina ya ***Nevirapine*** *(NVP) ya maji kwa watoto wachanga waliozaliwa na akina mama wenye maambukizi ya VVU, na asilimia 82 wana dawa za kupunguza makali ya maambukizi.*

***Kwa mawasiliano zaidi:***
*Mkurugenzi Mkuu*
*Ofisi ya Taifa ya Takwimu*
*18 Barabara ya Kivukoni*
*S.L.P 796,*
*119921 , Dar es Salaam*
*Tanzania.*

*Simu: +255 22 2122722/3, +255 22 2122724;*
*Nukushi: +255 22 2130852;*
*Barua pepe: dg@nbs.go.tz.;*
*Tovuti www.nbs.go.tz.*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# Utafiti wa Tathmini ya Utoaji wa Huduma za Afya Tanzania (TSPA) 2014/15





## UTANGULIZI

Utafiti wa Kutathmini Utoaji wa Huduma za Afya Nchini Tanzania (TSPA) wa mwaka 2014-15 ni wa pili kufanyika nchini. Utafiti wa kwanza ulifanyika mwaka 2006. Utafiti ulikusudia kukusanya taarifa kutoka katika sampuli ya vituo vyote vinavyotoa huduma ya afya nchini na kuangalia utayari wa vituo hivyo kutoa huduma bora ya afya ya mtoto, uzazi wa mpango, afya ya uzazi na mtoto mchanga, VVU, magonjwa yatokanayo na ngono, magonjwa yasiyoambukiza na kifua kikuu.

Utafiti wa TSPA wa mwaka 2014-15 ulihusisha sampuli ya vituo vya kutolea huduma za afya vinavyofikia 1,200 kutoka katika mikoa yote ya Tanzania. Kati ya vituo 1,200 vilivyochaguliwa kushiriki katika utafiti, vituo 1,188 vilifanikiwa kutembelewa.Matokeo ya Utafiti wa TSPA ya mwaka 2014-15 yanapatikana kwa aina ya kituo, mamlaka inayoendesha kituo husika na katika mikoa yote 30 ya Tanzania (mikoa 25 kwa Tanzania Bara na mikoa mitano (5) kwa Zanzibar).

Malengo ya TSPA 2015

- Kuangalia kiwango cha utayari au uwezo wa vituo vya afya katika kutoa huduma bora za afya;
- Kutambua upungufu unaokwamisha utoaji wa huduma bora za afya;
- Kutoa taarifa za msingi juu ya uwezo wa vituo vya afya katika utoaji wa huduma mbalimbali za afya zikiwemo za VVU/UKIMWI


**Idadi ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya vilivyotembelewa katika utafiti wa TSPA wa mwaka 2014-15: Kwa aina na Umiliki wa kituo husika**

Aina ya Kituo:
Hospitali: Idadi=256
Kituo cha Afya: Idadi=379
Zahanati: Idadi =493
Kliniki: Idadi =60

Umiliki wa vituo:
Serikali: Idadi =780
Binafsi (biashara): Idadi =184
Shirika la Umma: Idadi =20
Asasi ya Kidini: Idadi =204

## Matokeo Muhimu TSPA 2015:

## Huduma za Afya ya Mtoto




Takriban vituo vyote nchini (asilimia 98) vinatoa huduma ya tiba kwa watoto wanaougua, asilimia 81 ya vituo vyote nchini vinatoa chanjo kwa watoto na asilimia 84 ya vituo huduma ya ufuatiliaji mwenendo wa ukuaji wa mtoto. Vituo vinane kati ya 10 vinavyotoa huduma za afya nchini, vinatoa pia huduma tatu za msingi kwa afya ya mtoto. Zaidi ya asilimia 80 ya hospitali na vituo vya afya zinatoa huduma zote tatu kwa 2 ukilinganisha na mwaka 2006.

## Huduma za Uzazi wa Mpango

Huduma za kisasa za uzazi wa mpango zinapatikana kwa

asilimia 80 ya vituo vyote vinavyotoa huduma za afya nchini.

Matokeo haya yanaonyesha ongezeko la asilimia nne (4),


ikilinganishwa na asilimia 76 ya utoaji huduma za kisasa za uzazi wa mpango kwa utafiti wa mwaka 2006. Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2015 karibu vituo vyote vya serikali (97%) vinatoa huduma za uzazi wa mpango ikilinganishwa na asilimia 35 ya vituo binafsi vya kibiashara na asilimia 41 ya vituo vinavyomilikiwa na asasi za kidini. Utafiti huu unaonesha kuwa asilimia 81 ya vituo vya afya na zahanati zinatoa huduma za uzazi wa mpango.

## Huduma za Afya ya Uzazi

Upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi ni wa uhakika nchini kote. Zaidi ya vituo 8 vya afya kati ya 10 nchini vinatoa huduma kwa wajawazito. Hospitali na vituo vya afya vinaongoza kwa kutoa huduma ya Afya ya uzazi (asilimia 91 kila kimoja). Asilimia 85 tu ya zahanati sawa na wastani wa kitaifa kwa vituo vyote kutoa huduma za wajawazito.

Vituo vya afya vinavyomilikiwa na Serikali na vile vya mashirika ya dini, ndiyo yenye kiwango kikubwa cha utoaji wa huduma kwa wajawazito (asilimia 97 na asilimia 81), ikilingalishwa na kiwango cha asilimia 36 ya vituo vinavyomilikiwa na watu au mashirika ya binafsi.

Upatikanaji wa huduma kwa wajawazito unatofautiana kutoka mkoa mmoja hadi mwingine. Asilimia 43 tu ya vituo katika mikoa ya Mjini Magharibi na asilimia 52 tu ya vituo vya Dar es Salaam vinatoa huduma kwa wajawazito, ikilinganishwa na vituo vyote katika Mikoa ya Lindi.




Kwa vituo vinavyotoa huduma kwa wajawazito, asilimia 83 ya vituo hivi vina kipimo cha malaria cha papo kwa hapo (Malaria RDT), vile vile vituo vinavyotoa huduma kwa wajawazito, asilimia 30 ya vituo hivi vina kipimo cha kupima wingi wa damu .